*Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), 82-99*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.6

# Mawanda ya Taaluma za Ukalimani na Tafsiri na Haja ya Kuboresha Ufundishaji Wake

*Titus Mpemba*[1]

**Ikisiri**

Umuhimu wa ukalimani na tafsiri umeongezeka kutokana na utandawazi. Wakalimani na wafasiri wengi wamekuwa wakiandaliwa ili kuendana na kasi ya ongezeko la mahitaji ya wakalimani na wafasiri. Kutokana na kasi ya ongezeko hili, na uhaba au ukosefu wa walimu wabobevu wa ukalimani na tafsiri, walimu wa lugha ambao tafsiri na ukalimani si nyuga zao za ubobevu wamejikuta wakipewa majukumu ya kufundisha kozi za ukalimani na tafsiri vyuoni. Matokeo yake, walimu hao wamekuwa wakihangaika kufikiria mambo ya kufundisha. Kwa kuwa ukalimani na tafsiri si nyuga walizobobea, hujikuta wakifundisha juujuu. Wahitimu wanaotokana na ufundishaji wa juujuu huwa hawajapikwa sawasawa lakini hutazamiwa kuwa walimu wa baadaye wa ukalimani na tafsiri vyuoni. Aidha, huchukuliwa kuwa wamesomea kozi hizo. Kutokana na kutoandaliwa vyema, hujikuta wanaishia kuchukua miongozo ya kozi waliyotumia enzi za uanafunzi wao. Kisha, huhawilisha kwa kiasi kikubwa yale waliyofundishwa na mwalimu mwanzilishi wa kozi na kuyarithisha kwa vizazi vingine bila kuongezewa vionjo vya kibunifu kuendana na mabadiliko na mazingira ya soko. Hivyo, ufundishaji huwa wa kimazoea zaidi. Kwa hiyo, kuna haja ya wanataaluma kubadilishana uzoefu miongoni mwao, kukumbushana kuhusu mabadiliko yanayotokea na kuboresha zaidi ufundishaji wa nyuga hizi. Makala hii imelenga kutimiza azma hii kwa kujielekeza katika maarifa ya kibiashara kama kionjo kinachohitaji kuongezwa katika mitalaa ya ukalimani na tafsiri vyuoni ili kuboresha ufundishaji wa nyuga madhukura. Hususani, makala inatilia mkazo elimu ya huduma kwa wateja na uandaaji wa nyaraka za kibiashara. Makala inasisitiza kuwa, kutokana na umuhimu wake, elimu ya huduma kwa wateja haina budi kuongezwa katika mitalaa ya ukalimani na tafsiri.

## 1.0 Utangulizi

Katika maisha ya binadamu, ukalimani na tafsiri ni desturi zinazosemekana kuwapo tangu kale (Pöchhacker, 2009, 2016; Giambruno, 2008; Baker na Saldanha, 2009; Wanjala, 2011). Ingawa kuna wanaoona kuwa kuingia kwa wageni katika bara la Afrika “pamoja na hati ya maandishi ya Kiarabu na baadaye ya Kirumi” ndiko kulikozua haja ya taaluma ya tafsiri (Ngugi, 2012),

[1] Mhadhiri, Idara Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: mpembatitus@gmail.com

Baker na Saldanha (2009) wanaona kuwa shughuli za ukalimani na tafsiri katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara "zina umri takribani sawa na mawasiliano kwa njia ya mdomo". Pamoja na shughuli hizo kuwa na umri mkubwa Afrika, taaluma za tafsiri na ukalimani katika Ukanda wa Afrika Mashariki zingali changa (Ryanga, 1985). Ijapokuwa uchanga huo umezungumziwa tangu miaka ya 1980, hali hii haijabadilika sana. Hata hivyo, kutokana na utandawazi, umuhimu wa ukalimani na tafsiri umeongezeka na unazidi kuongezeka (Pérez-González na Susam-Saraeva, 2012; Mahero na Kandagor, 2020). Wakalimani na wafasiri wengi hivi sasa wanaandaliwa ili kuendana na kasi ya ongezeko la mahitaji ya wakalimani na wafasiri (Mpemba, 2013; Mahero na Kandagor, 2020). Pamoja na hayo, kuna changamoto kadhaa zinazoyumbisha ufundishaji wa taaluma hizo, kubwa ikiwa uhaba wa walimu wabobevu wa nyuga hizo kama anavyothibitisha mwalimu mmoja wa Kiswahili katika chuo kikuu kimoja nchini Tanzania:

> Huku nafundisha kozi hiyo [ya Ukalimani na Tafsiri] kwa kuwa **hakuna mtu aliyebobea katika uga huo**. Mimi ... nimeisoma kozi ya tafsiri peke yake semesta moja nikiwa nasoma shahada ya kwanza ... (Mawasiliano binafsi baina ya mtafiti na mtoataarifa, tarehe 08 Juni 2019; msisitizo, mabano mraba na taarifa zilizomo ni zangu.)


Dondoo hili linaonesha kuwa, kutokana na kasi ya ongezeko la umuhimu wa ukalimani na tafsiri, walimu wa lugha wasio wabobevu wa tafsiri na ukalimani wamekuwa wakipewa majukumu ya kufundisha kozi hizo vyuoni. Jambo hili linaelezwa pia na Al-Jarf (2008) kutokea huko Saudi Arabia. Ingawa hakuna utafiti uliochunguza matokeo ya walimu wasio wabobevu kupewa jukumu la kuandaa na kufundisha kozi wasizozimudu, tunaamini kuwa huhangaika na kufadhaika. Hivyo, tunadai kuwa hujikuta wakifundisha ili kutimiza tu wajibu na, hatimaye, kutoa wahitimu wasioiva barabara. Wahitimu hawa huhesabiwa kuwa wamesomea nyuga hizo na huwa walimu wake vyuoni baadaye kama tulivyoona katika dondoo hapo juu. Kwa kuwa hawakuandaliwa vizuri, wahitimu hawa wanapokuwa walimu, kama tutakavyoonesha baadaye, aghalabu huchukua miongozo ya kozi waliyotumia enzi za uanafunzi wao, kukiendeleza walichofundishwa na walimu waanzilishi wa kozi hizo na kukirithisha kwa vizazi vingine bila kubuni vionjo vipya vinavyoendana na mabadiliko na mazingira ya soko. Hiyo, tunaweza kudai kuwa uandaaji wa wakalimani na wafasiri aghalabu umekuwa ukifanyika kimazoea.

Kwa hiyo, makala hii inachunguza ufundishaji wa taaluma za ukalimani na tafsiri katika vyuo vikuu teule vya Tanzania ili kubaini ni uga upi unasisitizwa zaidi katika mafunzo. Kisha, makala inapendekeza kuwa mitalaa ya mafunzo ya tafsiri na ukalimani izingatie nyuga tumizi kama vile maarifa ya utumiaji wa kamusi, maarifa ya utumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)

na maarifa ya kibiashara kama vionjo vipya vinavyohitajika sasa katika mitalaa ya ukalimani na tafsiri vyuoni. Kwa sababu si rahisi kuzungmzia nyuga zote tumizi katika makala moja, makala inatumia kielelezo cha maarifa ya kibiashara tu ikitilia mkazo elimu ya huduma kwa wateja na stadi za kuandaa nyaraka za kibiashara kama vile ankara. Kutokana na umuhimu wake, makala inasisitiza kuwa elimu hii itolewe kwa wanafunzi wa ukalimani na tafsiri kama sehemu ya mtalaa.

## 2.0 Mawanda ya Taaluma za Ukalimani na Tafsiri

Miongoni mwa wanazuoni wanaojulikana kwa kufanya kazi kubwa kuhusu ubainishaji wa kina wa mawanda ya taaluma za ukalimani na tafsiri ni Holmes (1984/2004) na Toury (1995). Wanazuoni hao wanayaweka mawanda hayo katika makundi ya nyuga mbili, yaani nyuga menyu na nyuga tumizi kama zinavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1:




***Kielelezo Na. 1: Nyuga Menyu na Nyuga Tumizi za Taaluma za Ukalimani na Tafsiri***

**Chanzo:** Mtafiti, kutokana na mawazo ya Munday (2012)

Kama Kielelezo Na. 1 kinavyoonesha, **nyuga menyu** na **nyuga tumizi** ndiyo **maeneo makuu** ya **tafiti** na **ufundishaji** wa taaluma za ukalimani na tafsiri, kila eneo likiwa na malengo yake mahususi. Malengo makuu ya **nyuga menyu** ni (1) kuelezea au kufafanua masuala mbalimbali ya ukalimani na tafsiri, (2) kuweka misingi ya jumla ya kikanuni inayoweza kuelezea na kutabiri masuala hayo, na (3) kutoa ufafanuzi kuhusu jinsi mambo mbalimbali ya ukalimani na tafsiri yalivyo. Malengo ya **nyuga tumizi** ni kutumia maarifa ya nyanja mbalimbali katika shughuli za ukalimani na tafsiri. Kwa mfano, nyuga tumizi hutumia maarifa ya usanifu wa mitalaa na mbinu za ufundishaji na tathmini katika mafunzo ya wakalimani na wafasiri. Kadhalika, nyuga tumizi hutumia maarifa ya vitendea kazi kama vile kamusi na nyenzo zingine zinazosaidia kufanya kazi za tafsiri na

ukalimani, mathalani, TEHAMA na ujuzi wa wataalamu wa nyanja mbalimbali. Nyuga tumizi pia hutumia maarifa ya uandishi na uhariri, maarifa ya uhakiki wa ubora wa kazi za tafsiri na ukalimani, maarifa ya kibiashara na kijasiriamali, uundaji wa istilahi (teminografia) na stadi za mawasiliano. Mwisho, nyuga tumizi huzingatia maadili na itikeli za kazi. Yote haya hufanyika ili kurahisisha au kuboresha utendajikazi. Malengo ya (1) na (2) ya nyuga menyu za tafsiri na ukalimani hushughulikiwa katika nyuga za kinadharia na lile la (3) hushughulikiwa katika nyuga za kiufafanuzi.

Nyuga za kinadharia zinahusu misingi ya jumla ya kikanuni inayowekwa ili kuelezea na kutabiri masuala mbalimbali ya kikalimani na kitafsiri. Misingi hiyo huitwa **nadharia za ukalimani na tafsiri**. Nadharia zinaweza kuwa ***za jumla*** au ***mahususi***. Nadharia ***za jumla*** zinajaribu kuelezea kila aina ya ukalimani au tafsiri na kutoa majumuisho yanayoweza kuwa maujudi kwa ukalimani na tafsiri kwa jumla (Munday, 2012). Nadharia ***mahususi*** zinajihusisha na – au zinajibana katika – masuala fulani mahususi. Kwa mfano, nadharia za jumla zinaweza kuwa *za neno kwa neno, maana kwa maana, uhemenyuti, usawe na athari sawa,* na *nadharia ya skopos.* Nadharia mahususi zinaweza kuangalia *njia fulani za mawasiliano.* Kwa mfano, ukalimani au tafsiri ya **lugha za alama**, **ndimi/lugha za mizimu**, **soga za mitandaoni**, **mashine**, na **vyombo vya habari,** kama vile matangazo ya biashara magazetini, redioni na runingani na sikikeolwa[2]). Nadharia mahususi zinaweza pia kuangazia *maeneo fulani* ya kijiografia (kwa mfano, ukalimani au tafsiri ya lugha za Kichina na Kikorea), *aina fulani za matini* (kwa mfano, ukalimani au tafsiri ya **matini za kiufundi**, **kawaida**, **kisheria/kimahakama**, **kifasihi**, na **kisayansi**), *kipindi fulani* (kwa mfano, ukalimani au tafsiri katika **kipindi cha kabla ya ukoloni** au **kipindi cha ukoloni** n.k.). Vilevile, nadharia mahususi zinaweza kuangazia *matatizo fulani* (kwa mfano, **matatizo ya kiutendaji** katika ukalimani mikutanoni, changamoto za **kuteua visawe mwafaka** wakati wa kutafsiri matini za kitamaduni) au *ngazi fulani* (kwa mfano, ukalimani au tafsiri ya **neno** kwa **neno** au **sentensi** kwa **sentensi**, na ukalimani au tafsiri kama uzalishaji wa **vilongo**).

Nyuga za kiufafanuzi, kwa upande mwingine, huchunguza na kufafanua *mchakato* wa kukalimani au kufasiri, *matokeo* ya kukalimani au kufasiri na *uamilifu* au *dhima* ya kazi ya tafsiri au ukalimani. Uchunguzi wa mchakato wa kukalimani au kufasiri huhusu saikolojia ya ukalimani au tafsiri. Hivi ni kusema, huchunguza yale yatokeayo katika akili ya mkalimani au mfasiri. Uchunguzi wa matokeo ya kukalimani au kufasiri huhusu natija inayopatikana baada ya mchakato

---

[2] Istilahi hii imeundwa na mwandishi kwa kuambatanisha maneno *sikike* (inayosikika) na *olwa* (inayoonwa) ili kuwakilisha istilahi ya Kiingereza ya *audiovisual*.

wa kukalimani au kufasiri. Ikisemwa vinginevyo, uchunguzi huu huhusu natija zilizopo tayari. Kwa mfano, mtafiti anaweza kuchunguza tafsiri za karne ya 19 kutoka Kijerumani kwenda Kiswahili na kuzilinganisha na za karne ya 21 katika lugha hizo ili kuona kama kuna mabadiliko yoyote au kama kuna mbinu mpya. Uchunguzi wa uamilifu au dhima ya kazi ya tafsiri au ukalimani huhusu ufafanuzi wa jinsi kazi ya tafsiri au ukalimani ilivyokidhi utamaduni au matarajio ya jamii lengwa au hadhira lengwa. Hapa, mtafiti hujihusisha zaidi na miktadha ya tafsiri na ukalimani. Kwa mfano, anaweza kuangalia ni matini gani zilitafsiriwa lini kwa lugha gani na athari yake ilikuwa ipi. Mathalani, anaweza kuangalia jinsi tafsiri za 'Sinema za Bongo' kwa Kiingereza zinavyozingatia au kupotosha kanuni ya athari sawa na jinsi tafsiri hizo zinavyokubalika kwa watazamaji waliokusudiwa kusaidiwa kimawasiliano na tafsiri hizo.

Ili mhitimu wa masomo ya tafsiri na ukalimani aive barabara, hana budi kupata mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia mawanda yote yaliyofafanuliwa. Je, hali ikoje kwa wanaojifunza tafsiri na ukalimani Afrika Mashariki?

## 3.0 Ufundishaji wa Ukalimani na Tafsiri Afrika Mashariki

Katika Ukanda wa Afrika Mashariki, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2005 iliingiza mada za ukalimani na tafsiri katika mihtasari ya masomo ya Kiswahili na Kiingereza kwa kidato cha tano na cha sita (Mpemba, 2013, 2015). Tukiondoa juhudi hizi, utafiti huu unaonesha kuwa ufundishaji wa masomo ya ukalimani na tafsiri katika nchi madhukura aghalabu hufanyika katika ngazi ya chuo kikuu. Hata hivyo, vyuo vinavyotoa mafunzo ya ukalimani na tafsiri kama masomo ya utaalamu mahususi ni vichache (Mpemba, 2013). Mathalani, nchini Kenya, Chuo Kikuu cha Nairobi ndicho hufanya hivyo kupitia Kituo cha Tafsiri na Ukalimani. Katika kituo hicho, tafsiri hufundishwa kuanzia ngazi ya umahiri hadi uzamivu, na ukalimani vivyo hivyo. Nchini Tanzania, Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro na Chuo Kikuu cha Dodoma ndivyo pekee hufunza na kutoa vyeti katika taaluma za ukalimani na tafsiri kama nyuga mahususi. Kwa sababu ya uchache wa vyuo vya mafunzo ya wataalamu wa ukalimani na tafsiri, kuna uhaba wa wataalamu waliojihususisha na masomo haya na kupata vyeti vya utaalamu wa nyuga hizi kama vile astashahada ya ukalimani, astashahada ya tafsiri, stashahada ya ukalimani, stashahada ya tafsiri na shahada ya ukalimani.

Vyuo vingi vya nchi za Afrika Mashariki hufunza kiasi tu cha maarifa ya nyuga za ukalimani na tafsiri. Tukichunguza ufundishaji wa masomo ya nyuga za ukalimani na tafsiri unavyofanyika katika vyuo vikuu mbalimbali, yanabainika mambo makuu mawili. Mosi, taaluma hizi aghalabu hazijapewa hadhi

zinayostahili. Hizi ni taaluma mbili zinazojitegemea (Garzone na Viezzi, 2002; Pöchhacker, 2004; Mpemba, 2013) lakini katika vyuo vingi hufundishwa kwa kuunganishwa kama kozi moja, huku kipengele cha tafsiri kikipewa nafasi kubwa. Kwa mfano, nchini Uganda, Chuo Kikuu cha Makerere, Chuo Kikuu cha Kyambogo na Chuo Kikuu cha Kiislamu hufundisha ukalimani na tafsiri kama kozi moja ya mwaka wa pili, huku kipengele cha tafsiri kikipewa msisitizo zaidi. Mwalimu wa somo hilo katika chuo kimojawapo alithibitisha hili alipozungumza na mwandishi wa makala hii akisema:

> Hapa tunafundisha [ukalimani na tafsiri] kama kozi [moja] tu kwa wanafunzi wa mwaka wa pili. Lakini [kipengele] cha tafsiri ndicho kinasisitizwa zaidi. Chuo [Kikuu] cha Kyambogo pamoja na cha Kiislamu cha IUIU [*Islamic University in Uganda*] pia vinafundisha. (Mawasiliano binafsi baina ya mwandishi na mtoataarifa, tarehe 12 Juni 2018; mabano mraba na taarifa zilizomo ni yangu.)

Uchunguzi wa miongozo ya ufundishaji kutoka vyuo mbalimbali nchini Tanzania umeonesha kuwa hali hii pia inajitokeza katika vyuo vingi nchini. Mathalani, katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agostino (mabewa yake yote), masomo ya ukalimani na tafsiri hufundishwa yakiwa yameunganishwa katika kozi moja ya mwaka wa pili (**SW 240: Ukalimani na Tafsiri**), huku kipengele cha tafsiri kikisisitizwa zaidi. Kati ya mada tano za kozi hii, ukalimani unajitokeza kwa kiasi kidogo tu katika mada mbili[3]. Katika vyuo vingine, tafsiri peke yake ndiyo hufundishwa, huku kipengele cha ukalimani kikidokezwa tu au kikiachwa kabisa. Kwa mfano, katika Chuo Kikuu Mzumbe, kuna kozi moja ya tafsiri kwa mwaka wa tatu (**KSW 302: Nadharia ya Tafsiri na Uchanganuzi)**. Katika mwongozo wa kozi hiyo, ukalimani unajitokeza mara moja tu katika moduli ya kwanza (**Utangulizi**) kama "***Dhana ya Ukalimani***". Aidha, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (Arusha) hufundisha tafsiri peke yake kama kozi ya mwaka wa pili (**LAN 207: Tafsiri: Nadharia na Vitendo**). Katika mwongozo wa kozi hii, wenye moduli zipatazo sita, ukalimani unajitokeza mara mbili tu. Katika moduli ya kwanza (**Nadharia ya Tafsiri**), kipengele cha 1.5, kuna mada ya "***Tafsiri na Ukalimani***" iliyokusudiwa kuonesha uhusiano baina ya tafsiri na ukalimani. Mahala pa pili panapojitokeza ukalimani ni katika moduli ya sita (**Upungufu katika Tafsiri na Ukalimani**) ambapo panaoneshwa sababu za upungufu katika tafsiri na ukalimani na mbinu za kuurekebisha. Kadhalika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hufundisha tafsiri peke yake kwa mwaka wa kwanza (***OSW 124: Theory***

[3] Ukalimani unajitokeza katika mada ya kwanza (Dhana za **Ukalimani**, Ukafsiri, Ufasili na Tafsiri) na ya tatu (Uhusiano wa **Ukalimani**/Tafsiri na Taaluma mbalimbali). Mada tatu zinazosalia zinahusu tafsiri peke yake, au tafsiri ikihusishwa na taaluma zingine.

***and Practice of Translation*)** na kwa mwaka wa pili (**OSW 134: Tafsiri – Nadharia na Mbinu**).

Inapotokea ukalimani na tafsiri zikafundishwa katika chuo kimoja kama kozi mbili au masomo mawili tofauti, basi somo la ukalimani au kozi ya ukalimani huwa haifundishwi kwa upana na kwa kina ikilinganishwa na somo au kozi ya tafsiri. Kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro, ukalimani na tafsiri hufundishwa kama masomo mawili yanayojitegemea yakiwa na kozi mbalimbali, huku kozi za tafsiri zikitawala kwa kuwa nyingi au kwa kuwa na mada nyingi zaidi. Akithibitisha hali hii, mhadhiri mmoja wa Chuo hicho alisema, "Tafsiri hupewa nafasi kubwa kuliko ukalimani" (mawasiliano binafsi baina ya mtafiti na mtoataarifa, tarehe 19 Septemba 2020). Aidha, mnamo mwaka 2017, Chuo Kikuu cha Dodoma kilianzisha shahada ya taaluma za ukalimani na tafsiri (mawasiliano binafsi baina ya mtafiti na mtoataarifa, tarehe 18 Mei 2021). Katika programu hiyo, kozi za tafsiri ni nyingi kuliko za ukalimani. Hata katika baadhi ya kozi zinazoziunganisha nyuga hizi, moduli za tafsiri ni nyingi kuliko zile za ukalimani.

Jambo la pili ni kwamba mwelekeo wa ufundishaji wa kozi hizi katika vyuo vingi umefuata mkondo wa kusisitiza 'nyuga menyu' za taaluma za ukalimani na tafsiri na kuzipuuza au kuzipa msisitizo hafifu 'nyuga tumizi' na maarifa mengine yanayoweza kusaidia kuboresha uandaaji wa wafasiri na wakalimani. Mifano ya maarifa hayo ni 'uandishi na uhariri', 'uundaji wa istilahi (teminografia)', 'utumiaji wa kamusi', 'stadi za mawasiliano', 'maadili na itikeli za kazi', 'biashara' na 'ujasiriamali'. Ili kuweza kulifuatilia suala hili kwa undani zaidi, mwandishi wa makala hii aliteua vyuo vikuu kumi na viwili na kukusanya miongozo ya ufundishaji inayotumika katika uandaaji wa wakalimani na wafasiri mbalimbali nchini Tanzania.

Ili kuweza kuvipata vyuo teule, kanda sita zilibainishwa: (1) Kanda ya Kaskazini, (2) Kanda ya Kati, (3) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, (4) Kanda ya Pwani, (5) Kanda ya Ziwa, na (6) Kanda ya Zanzibar. Kutoka katika kila Kanda, vyuo vikuu viwili viliteuliwa kwa kuzingatia ukubwa, ushiriki katika ufundishaji wa tafsiri na ukalimani na/au urahisi wa kupatikana kwa miongozo ya kufundishia masomo hayo. Kutoka Kanda ya Kaskazini, Chuo Kikuu cha Arusha na Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira viliteuliwa. Kutoka Kanda ya Kati, Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana cha Tanzania viliteuliwa. Kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Chuo Kikuu cha Iringa na Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji ndivyo viliteuliwa. Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa hakikuteuliwa kwa sababu ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho kiliteuliwa katika Kanda ya Pwani. Kutoka Kanda ya Pwani, viliteuliwa Chuo

Kikuu cha Dar es Salaam (Bewa Kuu la Mwalimu Julius Nyerere) na Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro. Kutoka Kanda ya Ziwa, mtafiti aliteua Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agostino (Bewa la Mwanza na Bewa la Bukoba). Na kutoka Kanda ya Zanzibar, mtafiti aliteua Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Sumait.

## 4.0 Mitalaa ya Ukalimani na Tafsiri katika Vyuo Vikuu Teule vya Tanzania

Uchunguzi wa miongozo ya kozi za tafsiri na ukalimani kutoka vyuo teule ulidhihirisha mambo makuu matano. Jambo la kwanza ni lile lililokwishaelezwa katika sehemu ya 3.0, yaani ufundishaji wa kozi za ukalimani na tafsiri katika vyuo vingi kusisitiza zaidi **ujuzi na umilisi wa nyuga menyu** na kutozipa uzito stahiki **nyuga tumizi**. Kati ya vyuo 12 vilivyochunguzwa, ni vyuo vinne tu (sawa na asilimia 33.33)—Chuo Kikuu cha Sumait-Zanzibar, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe, na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agostino—ndivyo hufundisha baadhi ya nyuga tumizi, ingawa ni kwa kiwango kidogo sana. Vipengele tumizi vinavyogusiwa kwenye miongozo ya kozi za vyuo hivi ni **usawidi na uhariri wa tafsiri** (Chuo Kikuu cha Sumait-Zanzibar), **uhakiki wa tafsiri** (Chuo Kikuu Mzumbe na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), **tathmini ya tafsiri**, **uundaji wa istilahi**, matumizi ya **teknolojia** na ya **zana zinazohusiana na kazi za tafsiri**, **itikeli za mfasiri** (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) na **uhusiano wa tafsiri na nyanja zingine** kama isimujamii, isimutumizi, falsafa na ulumbi (vyuo vingine).

Jambo la pili, kama ambavyo pia limekwishaelezwa katika sehemu ya 3.0, ni ufundishaji wa kozi hizi katika vyuo vingi kuupendelea sana uga wa tafsiri na kuupa fursa ndogo sana au kuunyima fursa kabisa ule wa ukalimani. Jambo hili limedhihirika katika miongozo takribani yote iliyochunguzwa, isipokuwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) hufundisha kozi tatu za tafsiri na tatu za ukalimani kama nyuga zinazojitegemea. Kozi mbili za tafsiri hutolewa katika ngazi ya shahada ya awali, moja kwa mwaka wa kwanza (**KI 114: Utangulizi wa Nadharia na Mbinu za Tafsiri**) na moja kwa mwaka wa pili (**KI 218: Tafsiri: Nadharia na Vitendo**), na kozi mbili za ukalimani hutolewa kwa ngazi hiyo, moja kwa mwaka wa kwanza (**KI 115: Utangulizi wa Nadharia na Mbinu za Ukalimani**) na nyingine kwa mwaka wa pili (**KI 215 Ukalimani: Nadharia na Vitendo**). Katika ngazi ya shahada ya umahiri, kozi moja ya tafsiri (**KI 606: Tafsiri-Nadharia na Vitendo**) na moja ya ukalimani (**KI 632: Nadharia na Mbinu za Ukalimani**) hutolewa.

Jambo la tatu ni kuwa maarifa yanayotolewa na chuo kilichoanzisha ufundishaji wa kozi hizi au maarifa aliyoyapata mhitimu katika chuo alichojifunza

aghalabu ndiyo yaleyale yanayoendelezwa na vyuo vingine anakoenda kufundisha kama mwalimu wa baadaye. Mathalani, uchunguzi wa miongozo unaonesha kuwa hata majina ya kozi yanafanana au yanaendanaendana katika vyuo vinavyofunza kozi hizi. Kwa mfano, kabla ya mwaka 2009, katika Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kulikuwa na kozi ya ***SW 240: Translation Theory and Analysis*** (Nadharia ya Tafsiri na Uchanganuzi). Jina hili liliendelezwa katika kozi iliyofundishwa mwaka wa tatu kati ya mwaka 2009 na 2016 (**KI 316: Nadharia ya Tafsiri na Uchanganuzi**) na iliyofundishwa katika ngazi ya umahiri katika kipindi cha miaka madhukura (***ML626*: *Translation theory and techniques*** [Nadharia ya Tafsiri na Mbinu]). Majina haya yanaendana na kozi ya **KSW302: Nadharia ya Tafsiri na Uchanganuzi** ya Chuo Kikuu Mzumbe na **OSW134: Tafsiri-Nadharia na Mbinu** ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Aidha, kozi ya ***OSW 124: Theory and Practice of Translation*** ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania inafanana na ya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (Arusha) (**LAN 207: Tafsiri: Nadharia na Vitendo**). Mbali na majina ya kozi, maudhui ya kozi hizi katika vyuo vingi pia yanafanana kwa kiasi kikubwa.

Jambo la nne linahusu msisitizo wa lugha zinazohusika katika uhawilishaji wa ujumbe. Uhawilishaji unaopewa msisitizo ni wa lugha ya kusemwa na ya kuandikwa tu. Katika miongozo ya kozi zote kwenye vyuo vyote, hakutajwi lugha ya alama itumiwayo na watu wenye ulemavu wa kusikia.

Jambo la tano na la mwisho ni ufundishaji wa kozi hizi kutotoa fursa kwa maarifa ya kibiashara. Katika miongozo yote iliyochunguzwa, miongozo miwili tu ya Chuo Kikuu cha Dodoma ndiyo inayodokeza suala la biashara katika mada kama *Payment-Related Problems* (matatizo yanayohusiana na malipo), *Buying and Arranging Tools* (kununua na kupanga zana), *Cost Implication* (suala la gharama), *Starting a Business of Translation and Interpretation* (kuanzisha biashara ya tafsiri na ukalimani), na *Marketing and Developing Translation and Interpretation services* (kutafuta masoko na kustawisha huduma za tafsiri na ukalimani). Kwa kuzingatia mwelekeo wa serikali nyingi kusisitiza wahitimu wawe wafua-ajira na si watafuta-ajira, makala hii inatilia mkazo nafasi ya maarifa ya kibiashara katika uandaaji wa wakalimani na wafasiri. Vyuo vinavyofundisha kozi za ukalimani na tafsiri havina budi kulishughulikia suala la maarifa ya kibiashara, miongoni mwa maarifa mengineyo nyeti, katika kuwaandaa wafasiri na wakalimani. Dai kuu hapa ni kwamba ukalimani na tafsiri ni biashara ambayo inaendesha, na itaendelea kuendesha, maisha ya wahitimu mbalimbali. Hivyo, mafunzo yake hayana budi kuimarishwa na kujumuisha vipengee vya maarifa ya kibiashara.

## 5.0 Nafasi ya Nyuga Tumizi za Ukalimani na Tafsiri: Mfano wa Maarifa ya Kibiashara

Katika sehemu zilizotangulia, imeonekana kwamba mwelekeo wa ufundishaji wa kozi za ukalimani na tafsiri katika vyuo vingi aghalabu unasisitiza 'nyuga menyu' na kuzipuuza ama kuzipa msisitizo hafifu 'nyuga tumizi' kama vile 'utumizi wa nyenzo za mfasiri na mkalimani', 'uundaji wa istilahi (teminografia)', 'stadi za mawasiliano' na maarifa mengineyo kama vile 'uandishi', 'maadili na itikeli za kazi', 'biashara' na 'ujasiriamali'. Kwa sababu hiyo, tunapendekeza kuwa wabobezi wa ukalimani na tafsiri wawe wanafanya tafiti za mara kwa mara na kisha semina na warsha za mara kwa mara ili kushirikishana matokeo ya tafiti zao na kubadilishana uzoefu na walimu wa nyuga hizo kwa lengo la kufahamishana, miongoni mwa mambo mengine, mawanda ya nyuga hizo na kukumbushana kuhusu mabadiliko yanayotokea. Makala hii imejaribu kuitimiza azma hii na inapendekeza kuwa nyuga tumizi zizingatiwe katika mitalaa ya tafsiri na ukalimani. Kwa sababu ya ufinyu wa nafasi, makala hii inafafanua umuhimu wa maarifa ya kibiashara miongoni mwa maarifa madhukura.

### 5.1 Dhana ya Biashara

Kwa lugha ya kawaida, biashara inachukuliwa kuwa ni shughuli ya kununua na kuuza bidhaa kwa faida (BAKIZA, 2010; Longhorn, 2011; TUKI, 2019; Needle na Burns, 2019). Kadiri ya uelewa wa kawaida, biashara haihusiki na ununuzi na uuzaji wa bidhaa tu, bali pia utoaji wa huduma. Hivyo, ni vyema pia kujumuisha kipengele hicho katika fasili na kuichukulia biashara kama shughuli ya kununua na kuuza bidhaa au huduma. Hata hivyo, tukichunguza vizuri, tutabaini pia kwamba biashara haijifungi kwenye kuuza bidhaa zinazonunuliwa pekee. Wakati mwingine, wauzaji huwa ndio wazalishaji wenyewe wa bidhaa au huduma wanazouza. Hivyo, ili muuzaji aweze kuuza, ni lazima ama anunue au azalishe bidhaa au huduma zake mwenyewe. Kwa hiyo, biashara ni shughuli ya kununua au kuzalisha na kuuza au kutoa bidhaa au huduma kwa nia ya kupata faida.

Kwa lugha ya kitaalamu, biashara ni mchakato uhusuo uhawilishaji wa umiliki wa bidhaa, mali, milki au huduma kutoka kwa mtu mmoja au asasi moja kwenda kwa mtu au asasi nyingine kwa makubaliano ya kubadilishana na mtu huyo au asasi hiyo bidhaa, mali, milki au huduma nyingine au fedha kwa kusudi la kujipatia faida (Boone na Kurts, 2019; Needle na Burns, 2019).

Katika makala hii, tunatumia neno biashara kwa maana ya kawaida ya kuzalisha au kununua na kuuza bidhaa au huduma kwa lengo la kujipatia kipato. Dai ni kuwa shughuli za ukalimani na tafsiri huhusisha miamala inayotajwa katika

fasili hizo hapo juu na, kwa hiyo, tunaziona kuwa ni biashara. Je, ni nduni zipi zinazipa nyuga za ukalimani na tafsiri sifa ya ubiashara?

### 5.2 Ubiashara wa Ukalimani na Tafsiri

Wataalamu wa masuala ya biashara (taz. Schmenner, 1986; Uddin na Akhter, 2012; Needle na Burns, 2019) wanataja nduni mbalimbali za biashara, kubwa zikiwa mbili. Kwanza, katika biashara, kuna pande mbili. Upande mmoja kuna muuzaji na upande wa pili kuna mnunuzi; upande wa muuzaji unaweza pia kuwa ndiye mzalishaji. Kwa hiyo, kama nduni mojawapo, biashara hujihusisha na uzalishaji, ununuzi na uuzaji wa bidhaa au huduma (Needle na Burns, 2019). Nyuga za ukalimani na tafsiri ni biashara kwa sababu zinazo pande hizi mbili za wauzaji ama wazalishaji na wanunuzi. Wakalimani na wafasiri huzalisha huduma zao au bidhaa zao zinazotokana na michakato ya kiakili na kuziuza kwa watu au asasi zingine. Kwa mujibu wa Needle na Burns (2019), nduni kuu ya pili ya biashara ni kwamba wauzaji wa bidhaa au watoaji wa huduma hulenga kubadilishana bidhaa au huduma zao na fedha au thamani ya fedha kutoka kwa wanunuzi kwa minajili ya kujipatia faida au kipato. Kwa kuzalisha bidhaa zitokanazo na michakato ya kiakili na kuziuza kwa wanaozihitaji, wafasiri na wakalimani wanajipatia kipato cha kuendeshea maisha yao, jambo linalodhihirisha kwamba ukalimani na tafsiri ni biashara.

### 5.3 Kudumu katika Biashara ya Ukalimani na Tafsiri

Wahitimu wanaofuzu kozi za ukalimani na tafsiri vyuoni na kuingia sokoni ni wengi. Huko, hukutana na wataalamu wazoevu au wale wasio na utaalamu lakini wana uzoefu kwa kuhudumu kwenye tasnia za ukalimani na tafsiri kwa muda mrefu (Pérez-González na Susam-Saraeva, 2012). Kwa sababu hii, biashara hii ina ushindani. Hivyo, wanafunzi hawana budi kuandaliwa vyema ili kukabiliana na ushindani huo. Miongoni mwa mambo mengine, inabidi wapatiwe mafunzo ya kibiashara kuhusiana na mambo kadha wa kadha yatakayowawezesha kuendesha biashara yao kwa uthabiti. Hata hivyo, isivyo bahati, kama tulivyokwishaona, kipengele hiki kinakosekana ama hakisisitizwi katika mitalaa husika. Bila shaka, umefika wakati wa kubadilika sasa na kuacha kufundisha kwa mtindo wa kimazoea. Inafaa wanafunzi wafundishwe kulingana na mahitaji ya soko. Mathalani, kwa sababu ya ushindani, wanaweza kusaidiwa kujinusuru katika ushindani na kudumu katika biashara ya ukalimani na tafsiri kwa kuwafundisha jinsi ya kujitangaza na kushawishi wateja watake huduma zao. Aidha, kwa sababu watakabiliana na wateja mara kwa mara na kwa sababu watapaswa kuandaa nyaraka mbalimbali na kutunza kumbukumbu, wanaweza pia kufundishwa maarifa ya "huduma kwa wateja", "uandaaji wa nyaraka za kibiashara" na "utunzaji wa kumbukumbu". Haya ni baadhi tu ya maarifa ya kibiashara yanayoweza

kufundishwa kwa wanafunzi wa ukalimani na tafsiri. Kila mhadhiri hana budi kuwa mchunguzi, mtunduizi na mbunifu, jambo litakalofanya kozi ziwe hai na zenye kuvutia wanafunzi wengi na kukidhi mahitaji ya jamii kila wakati. Hivyo, ni muda mwafaka wa kuingiza vipengee vya maarifa ya kibiashara na nyuga zingine tumizi katika mitalaa kwa sababu maarifa hayo ni muhimu kama inavyodokezwa katika sehemu zinazofuata.

### 5.3.1 Kujitangaza

Biashara yoyote ile huhitaji wateja. Ili biashara iweze kustawi na kuendelea vizuri, inapaswa kuwa na wateja ambao upatikanaji wao utakuwa endelevu. Upatikanaji wa wateja unaweza kuwa endelevu na unaweza kuongezeka kama tu wateja wengi wataifahamu biashara hiyo na manufaa yake kwao. Wateja wanaweza kuifahamu biashara ikiwa mfanyabiashara atataingaza. Utangazaji wa biashara huwasaidia wateja kujua taarifa kama huduma zinazotolewa na mfanyabiashara husika, mahali anapopatikana, bei zake na kadhalika. Kwa sababu hii, Waswahili husema, “Biashara matangazo”. Bila kujitangaza, mfanyabiashara hatajulikana na anaweza kukumbwa na tufani ya mabadiliko na kutoweka sokoni. Hivyo, walimu hawana budi kuwafundisha wanafunzi mikakati ya kujitangaza ili waweze kukabiliana na ushindani wa kibiashara.

### 5.3.2 Huduma Bora kwa Wateja

Wateja wakishapatikana, wataendelea kuja kupata huduma ya mfanyabiashara husika na kuleta wateja wengine kama tu kuna huduma bora kwa wateja (Skogland na Siguaw, 2004; Uddin na Akhter, 2012). Huduma kwa wateja ni mfululizo wa shughuli unaolenga kumhudumia mteja kabla ya wakati wa au baada ya kununua bidhaa au huduma anayoihitaji. Mlolongo wa shughuli hizi hulenga kumridhisha mteja kwa kukidhi matarajio yake. Kwa hiyo, upatikanaji na uendelevu wa wateja hutokana na wateja hao kuridhishwa na huduma wanazopatiwa, kuanzia wanavyopokelewa, jinsi mawasiliano yanavyofanyika baina yao na mtu anayewahudumia mpaka wanavyopokea zao la mwisho la huduma wanayoihitaji au hata baada ya hapo.

Kama mfanyabiashara, mkalimani na mfasiri anatakiwa ajue jinsi ya kuhudumia vizuri wateja wake. Hana budi kuwasiliana nao vizuri na kwa ufanisi. Mathalani, mkalimani au mfasiri anawajibika kumjulisha mteja wake kuhusu mambo mbalimbali yanayoweza kuleta misuguano. Kwanza, mkalimani au mfasiri anatakiwa *kuwajulisha wateja jinsi kazi za kukalimani na kufasiri zinavyofanyika.* Ukalimani na tafsiri ni nyuga za kitaaluma na kitaalamu lakini watu walio wengi, ikiwa ni pamoja na baadhi ya wateja, hawaujui ukweli huu. Hivyo, hufikiri kuwa kila anayejua vyema lugha mbili au zaidi anaweza kukalimani au kufasiri kwa

ufanisi (Mlacha, 1996; Pérez-González na Susam-Saraeva, 2012). Kwa sababu hii, wateja wengi wanapomwendea mkalimani au mfasiri, huwa hawajaipa kazi hiyo uzito unaoistahili. Katika mazingira kama haya, mteja anaweza kumwendea mkalimani au mfasiri na hadidu za rejea ambazo hazitekelezeki kirahisi. Wateja hawa wanaweza kuelimishwa kwa lugha ya upole na ustaarabu ili waelewe kuwa ukalimani na tafsiri ni nyuga za kitaalamu na kitaaluma ambazo zina kanuni, taratibu na kaida zake. Mteja akilielewa hili atakubaliana na kaida hizo na atakuwa na uhusiano mzuri na mkalimani au mfasiri.

Pili, mkalimani au mfasiri *awajulishe wateja wake kuhusu kiwango cha muda uliokubaliwa kimataifa kukalimani au kufasiri kila kipande cha kazi (kwa mfano, saa tatu kwa siku, maneno thelathini kwa saa, saa nne kwa ukurasa au kurasa nne kwa siku, n.k.)*. Kwa sababu ya mawazo kama yaliyofafanuliwa hapo juu, baadhi ya wateja humwendea mkalimani au mfasiri na mashinikizo ya kumtaka afanye kazi kwa muda mrefu au mfupi kuliko kawaida kwa sababu wana haraka. Wateja wanatakiwa kujulishwa kuwa kuna utaratibu ambao ni wa kikaida ambapo mkalimani au mfasiri hawezi kuzidi kiwango cha saa fulani au kurasa fulani au maneno fulani kwa siku. Hivyo, inabidi wawe wavumilivu na wakubaliane na ukweli huo. Mkalimani au mfasiri asikubali kamwe kupokea kazi ambayo itamfanya amenyeke kuzidi kipimo na kujisababishia matatizo kama ya kiafya na kisaikolojia.

Tatu, mkalimani au mfasiri *awajulishe wateja mgawanyo wa kiasi cha fedha kinachotakiwa kwa kila kipande cha kazi (kwa mfano, kwa saa, kwa ukurasa, n.k)*. Wakalimani na wafasiri hawana budi kuwajulisha wateja wao kuwa kuna bei maalumu za kukalimani na kufasiri zilizoko sokoni na hivyo inabidi waziheshimu. Wawaeleweshe wateja kuwa ni kwa nini bei hizo zipo ili wajue kuwa hazikuzuka kivoloya. Wakalimani na wafasiri wanagenzi, na wakati mwingine hata wazoevu, hushawishika kupokea kazi ili wasizikose pesa zinazoambatana nayo, hata kama bei anayotaka mteja haiendani na viwango vilivyo sokoni. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kuiheshimu taaluma yao na miiko yake kwa kupokea kazi inayoendana tu na viwango vilivyopo sokoni. Watu hukiheshimu chako kama wewe mwenyewe utakiheshimu kwanza.

Jambo jingine linalopaswa kuzingatiwa katika kipengele cha huduma kwa wateja ni *usikivu kwa mteja*. Wateja huwa na matakwa yao mahususi kuhusiana na kazi wanayompatia mkalimani au mfasiri. Mkalimani au mfasiri anatakiwa kuwasikiliza wateja kuhusiana na matakwa hayo kama vile wangependa matokeo ya kazi ya ukalimani au tafsiri yawafae watu wa namna gani (kiwango cha elimu, utalaamu au ufundi, n.k.); mambo gani yaliyo kwenye matini chanzi yatokee pia au yasitokee kwenye matini lengwa (aina ya fonti, picha, vielelezo, n.k.). Ni

muhimu mkalimani na mfasiri ajue matakwa mahususi ya mteja wake ili aweze kuifanya kazi yake kikamilifu na kwa ufanisi. Matakwa ya mteja yanaweza kujumuisha **taarifa za masilugha** ambazo mkalimani au mfasiri anazihitaji ili kuufahamu muktadha wa matini chanzi na kuamua ni mbinu ipi ataitumia katika kufasiri au kukalimani matini chanzi (Munday, 2012). Hivyo, ni muhimu kwa mfasiri kuzifahamu taarifa kama hizi na kujua jinsi ya kuhusiana na mteja ili ikitokea taarifa hizo hazikutolewa, mkalimani au mfasiri amuulize mteja wake. Mathalani, mteja akitoa taarifa ya jumla kama vile "nina kazi yangu ya kukalimani/kufasiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili," na mkalimani au mfasiri akaacha kuulizia matakwa ya mteja wake, ukalimani au tafsiri itafanyika katika ombwe la kimuktadha (Munday, 2012).

Aidha, ili kuhakikisha kwamba mteja anaridhishwa na huduma anayopewa, mfasiri hana budi kuwa tayari kumsikiliza mteja wake hata baada ya kumaliza kazi. Kwa mfano, kama kuna makosa ya kiuchapaji au sentensi ambazo haziwasilishi ujumbe vizuri na zimempita mfasiri bila kuzigundua, basi awe tayari kushughulikia matatizo hayo kama mteja atayaleta. Hii ndiyo huduma nzuri kwa wateja ambayo walimu wanapaswa kuwafundisha wanafunzi.

### 5.3.3 Uandaaji wa Nyaraka za Kibiashara

Wanafunzi wa ukalimani na tafsiri hawana budi kufundishwa jinsi ya kuandaa nyaraka mbalimbali ambazo ni muhimu katika shughuli zao. Mathalani, ni muhimu kuwafundisha uandaaji wa *mapendekezo ya miradi*. Kwa sababu za ushindani wa kibiashara, wakalimani na wafasiri wanapaswa kuwa wabunifu. Wasisubiri kuletewa kazi. Wanatakiwa wajue pia kutengeneza fursa au kuzifua kazi hizo. Hivyo, wanatakiwa kuwa watunduizi. Wafanye tafiti wabainishe matatizo ya tafsiri na waandike mapendekezo ya kuyatatua matatizo hayo. Kwa mfano, mfasiri wa Kiswahili anaweza kuchunguza tafsiri mbalimbali za Kiswahili zilizofanywa kwenye programu mbalimbali za simu za mkononi kama NOKIA, SAMSUNG, n.k., na ukubalifu wake. Anaweza kubainisha umadhubuti na upungufu wake. Akishagundua upungufu huo, anaweza kuandika mapendekezo ya miradi ya jinsi ya kuziboresha zaidi programu hizo. Maarifa ya kufanya hivi hayapati kwingineko, bali kwa walimu wake na maktabani. Kwa hiyo, ni jukumu la walimu kuhakikisha kuwa mafunzo wanayotoa yanakuwa maujudi kwa wanafunzi kwa kuwapa nyenzo mwafaka zinazowawezesha kupambana vyema katika mazingira ya ushindani.

Waraka mwingine wa kibiashara ambao mkalimani na mfasiri anatakiwa kufahamu namna ya kuuandaa ni *ankara*. Ankara ni waraka wa kibiashara ambao huonesha muamala baina ya muuzaji na mnunuzi ukiorodhesha bidhaa

alizotumiwa au anazotumiwa mteja au huduma alizopatiwa au anazopatiwa, bei ya kila bidhaa/huduma na jumla ya fedha zinazodaiwa, tarehe, wahusika, taarifa za kodi au tozo nyinginezo zinazotakiwa kulipwa (kama zipo), punguzo na kadhalika. Panaweza pia kukawa na sehemu ya kutia saini. Kuna aina mbili za ankara: *ankara kifani* na *ankara halisi.* Ankara kifani hutumwa kwa mteja kabla hajapatiwa huduma ili ama akubaliane au asikubaliane na mtoa huduma, ilhali ankara halisi hutumwa baada ya bidhaa kutumwa au baada ya huduma kutolewa ili kumdai mteja alipie bidhaa au huduma hiyo. Ankara ni waraka muhimu sana katika miamala ya kibiashara. Kama wafanyabiashara, wakalimani na wafasiri hawana budi kufahamu jinsi ya kuuandaa. Mwandishi wa makala hii ameshuhudia wafasiri wengi, ambao ni wahitimu wa vyuoni, wanapoombwa ankara na wateja wao huishia kuduwaa kutokana na ukweli kwamba, licha ya kutojua kuiandaa, hawajui hata ankara ni kitu gani. Kwa hiyo, ni vyema kuingiza kipengele hicho katika mafunzo ya mkalimani na mfasiri ili kuwafunza wanafunzi jinsi ya kuandaa ankara halisi na ankara kifani.

Hizo ni baadhi tu ya nyaraka zinazoweza kuwanufaisha wanafunzi wakijua jinsi ya kuziandaa. Zipo na nyinginezo kama *bajeti*, *ripoti*, *kumbukumbu za hesabu* na kadhalika ambazo pia ni muhimu, lakini kwa sababu ya ufinyu wa nafasi, hatukuweza kuzifafanua hapa. Ni jukumu la kila mwalimu wa ukalimani na tafsiri kufikiria jinsi ya kuendana na wakati na mahitaji ya soko kwa kuingiza katika mafunzo yake maarifa ya kibiashara na nyuga zingine.

## 6.0 Hitimisho

Uandaaji wa wakalimani na wafasiri katika Ukanda wa Afrika Mashariki unakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo ya uhaba wa walimu wabobevu wa nyuga hizo. Hali hii imesababisha walimu wasio wabobevu kupewa jukumu la kuandaa na kufundisha masomo hayo au kozi hizo. Matokeo yake, ufundishaji umekuwa ukiendeshwa kimazoea zaidi ambapo maarifa ya waanzilishi wa kozi yameendelea kudumishwa na kurithishwa kizazi hadi kizazi kingine. Kwa sababu ya kutokuwa wabobevu, walimu walio wengi wameshindwa kuwa wabunifu. Eneo ambalo limeangaziwa katika makala hii kuwa limetelekezwa katika mafunzo ya mkalimani na mfasiri ni nyuga tumizi, hususani nafasi ya maarifa ya kibiashara. Makala hii imedai kuwa ukalimani na tafsiri ni biashara. Kwa sababu hiyo, kuna kila sababu na kila haja ya kujumuisha katika mitalaa ya mafunzo ya wakalimani na wafasiri maarifa ya kibiashara ili mafunzo yawe maujudi na yenye kukidhi hali ya ushindani sokoni. Hivyo, ni jukumu la walimu wanaofunza taaluma za ukalimani na tafsiri kuhakikisha kuwa jambo hilo linatekelezwa.

**Marejeleo**

Al-Jarf, R. (2008). “Benchmarks for Staffing Translation Departments in Saudi Arabia”. College of Languages and Translation 2nd Annual Meeting. King Saud University, Riyadh, Saudi Arabia. Aprili 26-30.

Baker, M. na Saldanha, G. (Wah.) (2008). *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. Abingdon/New York/Canada: Routledge.

Boone, L. na Kurtz, D. (2019). *Contemporary Business*. Hoboken, New Jersey: John Wiley & Sons, Inc.

Giambruno, C. (2008). “The Role of the Interpreter in the Governance of Sixteenth-and Seventeenth-Century Spanish Colonies in the ‘New World’: Lessons from the Past for the Present.” Katika C. Valero-Garces na A. Martin (Wah.), *Crossing Borders in Community Interpreting: Definitions and Dilemmas*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins Publishing Company. Kur. 27-50.

Mahero, T. na Kandagor, M. (2020). “Changamoto za Tafsiri katika Enzi ya Utandawazi.” *Mulika*. 39: 159-168.

Mlacha, A.K. (1996). “Dibaji” katika Mwansoko, Mekacha na Masoko (2013) *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Uk. v.

Mpemba, T. (2013). “Hali ya Taaluma ya Ukalimani Tanzania: Jana, Leo na Kesho.” *Kiswahili*. 76: 111-139.

Munday, J. (2012). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*. London/New York: Routledge.

Needle, D. na Burns, J. (2019). *Business in Context: An Introduction to Business and Its Environment*. London: Cengage Learning.

Ngugi, P.M.Y. (2012). “Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati.” *Mulika*, 31: 12-26.

Pérez-González, L. na Susam-Saraeva, Ş. (2012). “Non-professionals Translating and Interpreting: Participatory and Engaged Perspectives.” *The Translator*. 18(2): 149-165.

Pöchhacker, F. (2004). “I in TS: On Partnership in Translation Studies.” Katika C. Schäffner (Mh.) *Translation Research and Interpreting Research: Traditions, Gaps and Synergies*. Clevedon/Buffalo/Toronto: Multilingual Matters. Kur. 104-115.

Pöchhacker, F. (2009). “Issues in Interpreting Studies.” Katika J. Munday (Mh.) *The Routledge Companion to Translation Studies*. London/New York: Routledge. Kur. 128-140.

Ryanga, C.W. (1985). “Vitabu vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili.” *Kiswahili*, 52(1) &52(2): 161-174.

Schmenner, R.W. (1986). "How Can Service Businesses Survive and Prosper." *Sloan Management Review*. 27(3): 21-32.

Skogland, I. na Siguaw, J.A. (2004). "Are Your Satisfied Customers Loyal." *Cornell Hospitality Quarterly*. 45(3): 221-234. Inapatikana katika https://doi.org/10.1177/0010880404265231. Imesomwa tarehe 19 Aprili 2022.

TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Toleo la tatu, Nairobi: Oxford University Press East Africa Limited.

Uddin, M.B. na Akhter, B. (2012). "Determinants of Customer Satisfaction of Banking Industry in Bangladesh." *Pakistan Journal of Commerce and Social Sciences*. 6(2): 242-256.

Wanjala, F.S. (2002). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri: kwa Shule, Vyuo na Ndaki.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.